


Bibilia ya watoto  
Inawalettea

# Mwana Mpotevu



Kimeandikwa na: Edward Hughes

Kimeorodheshwa na: Alastair Paterson; Lazarus

Imerekebishwa na: Ruth Klassen; Sarah S.

Kimetafsiriwa na: Bethel Children's Home,  
Kisumu, Kenya and Emmanuel Menya


Kimedhibitishwa na: Bible for Children  
[www.M1914.org](http://www.M1914.org)

©2020 Bible for Children, Inc.


License: Kuna ruhusa ya kuchapa hadithi hii,  
lakini bila ya kuuza.



Yesu alipenda  
kuwaambia watu kuhusu  
msamaha wa Mungu.  
Lakini viongozi  
wa Kiyahudi  
walilalamikia  
urafiki Wake na  
wenye dhambi.



Hivyo Yesu alizungumzia  
hadithi tatu kuonyesha  
kwamba Mungu  
anafurahi  
wenye dhambi  
wanapohuzunikia  
dhambi zao.



Hadithi ya  
kwanza  
ilikuwa

kuhusu mtu  
mwenye  
kondoo  
mia. Mmoja  
akapotea.



Muda huohuo  
mchungaji  
akawaacha  
wale



tisini na tisa  
na kwenda  
kumtafuta  
yule  
aliyepotea.





Mchungaji  
alitafula mpaka  
akamuona kondoo  
aliyepotea. Kisha  
akamuweka  
mabegani na

kumrudisha  
nyumbani  
kwa furaha.





Akawaambia  
marafiki zake,  
"Furahini pamoja  
nami kwa maana  
nimempata  
kondoo wangu

aliyekuwa  
amepotea!"





Yesu akaeleza  
kwamba kuna  
furaha kuu  
mbinguni  
mwenye  
dhambi  
mmoja  
anapotubu.



Maana ya kutubu ni  
kuhuzunika kwa  
ajili ya dhambi  
zako -  
kuhuzunika  
kiasi cha  
kukufanya  
uziache!






Hadithi ya Yesu  
iliyofuata ilikuwa ya  
mwanamke aliyekuwa  
na sarafu kumi,  
pengine ilikuwa ni  
akiba ya maisha  
yake yote. Jambo  
baya likatokea.  
Akapoteza  
moja ya  
sarafu zake.



Akafagia! Akafagia!  
Akafagia! Mwanamke  
akaangalia kila mahali.



Hatimaye akaipata sarafu  
iliyopotea. Alifurahi sana.  
Unaweza kukisia kwamba  
alifanya nini? Ndiyo,  
aliwaambia

marafiki  
zake  
wote!





Yesu  
akasema  
tena, "Kuna  
furaha mbele  
ya malaika wa  
Mungu mwenye  
dhambi mmoja  
anapotubu."



Hadithi ya tatu  
aliyosimulia Yesu  
ilikuwa ya huzuni  
sana. Ilikuwa  
juu ya mvulana  
aliyeondoka  
kwenye  
nyumba  
ya baba  
yake.



Katika nchi ya mbali mvulana  
alitumia fedha yake kipumbavu.  
Angeweza kufanya nini baada ya

kuishiwa?




Mbaya zaidi, njaa  
ikaingia katika  
nchi ile. Mvulana  
angeweza  
kufa njaa.






Akiwa katika hali mbaya ya njaa, mvulana akapata kazi ya kulisha nguruwe. Lakini hakuna aliyempa chakula.



Alitamani kula chakula cha  
nguruwe. Labda alifanya hivyo!  
Mwishowe, fahamu za mvulana  
zikaarudi. Akatafakari, "Nyumbani,  
hata watumishi wanakula  
vizuri."






"Nitarudi nyumbani  
na kumwambia Baba  
najutia dhambi zangu.  
Sistahili kuwa  
mwana wake tena.  
Natumaini ataniajiri  
kama  
mtumishi."



Wakati mvulana bado yuko mbali na nyumbani kwao, baba yake akamuona anakuja. Kwa furaha, baba akamkimbia mwanae anayerudi


nyumbani. Akambusu mvulana na kumkumbatia.





“Baba, nimetenda dhambi. Sistahili kuwa mwana wako tena.” Mvulana alitaka kumuomba baba yake amujiri kama mtumishi.





Lakini baba  
akamkatisha.  
Leteni vazi  
bora, viatu, na  
pete kwa ajili  
ya mwanangu.  
Na andaeni  
sherehe  
kubwa.



Kulikuwa na sherehe ya  
ajabu kwa sababu  
mwana aliyekuwa  
amepotea  
ameonekana.



Yesu alisimulia hadithi hii kwa  
sababu inaonyesha  
jinsi Mungu  
anavyopenda  
kuwapokea  
wenye  
dhambi  
wanaotubu  
na kumjia.





Mwana Mpotevu

Hadithi kutoka kwa Neno la Mungu, Bibilia,

inapatikana katika

Luka 15

"Kufafanusha maneno yako kwatia nuru."

Zaburi 119:130



Mwisho



Hii hadithi ya bibilia  
inatueleza kumhusu Mungu wetu wa  
ajabu aliyetuumba na anayetaka tumjue.

Mungu anajua tumetenda mambo mabaya,  
anayoyaita dhambi. Adhabu ya dhambi ni  
mauti, lakini Mungu anakupenda sana hata  
akamtuma mwana wake wa pekee, Yesu, Ili  
afe msalabani na aadhibiwe kwa dhambi  
yako. Alafu Yesu akafufuka na kuenda  
nyumbani mbinguni! Ukimwamini Yesu na  
kumwomba msamaha kwa dhambi yako,  
Atakusamehe! Yesu atkuja na kuishi  
ndani yako, na utaishi naye milele.



Kama unaamini huu  
ni ukweli, Sema haya kwa Mungu:  
Mpendwa Yesu, ninaamini kuwa wewe ni  
Mungu, na ulifanyika mtu ili ufe kwa ajili  
ya dhambi zangu, ili niwe na maisha mapya,  
na siku moja nitaenda kuwa nawe millele.  
Nisaidie nikutii na niishi kwa ajili yako  
kama mtoto wako. Amina.

Soma bibilia na uzungumze na Mungu  
kila siku! Yohana 3:16

